ujenzi wa Kanisa hilo ndani ya kipindi cha miezi sita tu. Tulianza kuchangia ujenzi mwezi *Januari* na kukamilisha ujenzi mwezi *July, 2021*. Mara baada ya ujenzi huo kukamilika kwa ufanisi mkubwa, watu hao walivutiwa na huduma hiyo na hivyo baadhi yao walipendekeza kutovunjwa kwa kundi hilo la Whartsapp na badala yake iwe huduma endelevu ya ujenzi wa makanisa vijijini. Ni wakati huu pia tulipata ndugu *Bonifasi Nyamko* ambaye alivutiwa na kujiunga na kikundi chetu.



*Jengo la kanisa la TAG kurusanga likiwa limekamilika tarehe 05/09/2021*

Mara baada ya kupokea mapendekezo ya kutokuvunja kikundi, kilipita kipindi cha muda wa mwaka mzima toka mwezi **October, 2021** bila kufanya huduma yoyote ya ujenzi. Badala yake niliendelea kumwomba Mungu ili aseme na mimi kwa uhakika kama ni kweli iwe huduma au lilikuwa ni tukio la mara moja tu. Lakini pia, nilitaka kujua jinsi ambavyo pesa zitapatikana kwa ajili kuendeleza huduma ya kujenga makanisa na hasa ukizingatia kuwa huduma hii itahitaji fedha na upatikanaji wa fedha siyo jambo jepesi. Wakati huo huo nilikuwa naendelea kuandika kitabu kinachohusiana na utoaji wa sadaka.

Niliendelea na uandishi wa kitabu na wakati huo yale mapendekezo ya kuanzisha huduma ya ujenzi wa makanisa vijijini ni kama yalikuwa yamewekwa kapuni hivi. Mara baada ya zoezi la uandishi wa kitabu kukamilika, mwezi **Agosti, 2022** nilianza kufikiria juu ya sadaka ya shukrani nikatayotoa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuandika kitabu kinachohusu utoaji wa Sadaka. Napo ulipita muda mrefu bila kupata jibu la aina gani ya sadaka nitamtolea Mungu kwa kuniwezesha kuandika kitabu kwanza ndio mara yangu ya kwanza kuandika kitabu lakini pia ni kitabu cha Kiroho.

***Baadaye ndipo nilipata wazo kwamba ninaweza kufanya uzinduzi wa kitabu kwa njia ya kuitisha harambee na kisha fedha itakayopatikana kupitia hiyo harambee itumike kujenga makanisa vijijini***. Wazo hili lilipokuja ndipo nikakumbuka kuwa kuna